

## **MKATABA WA UPANGISHAJI.**

Umefanyika leo tarehe 01 Mwez February 2026 hadi tarehe 30 mwezi January 2031.

### **KATI YA**

**EMMANUEL MSIGWA** wa **Dar-es-salaam**, ambaye kwa madhumuni ya mkataba huu atajulikana kama **MWENYENYUMBA** kwa upande mmoja.

**NA**

**NDONYA GROUP** wa **Dar-es-salaam**, ambaye kwa madhumuni ya mkataba huu atajulikana kama **MPANGAJI**, kwa upande mwingine,

**KWA KUWA MWENYENYUMBA** ni mmiliki halali wa nyumba **Plot no 37049 ILALA, MSONGOLA** na anayo nia ya kuipangisha nyumba hiyo;

**NA**

**KWA KUWA MPANGAJI** anayo nia na yuko tayari kupanga nyumba hiyo,

### **BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIA YAFUATAYO:**

- (i) Kwamba kodi ya pango la nyumba hiyo itakuwa ni shilingi za Kitanzania elfu sabini (**TSH 70,000/=**) tu kila mwezi, itakayolipwa kwa mara moja.
- (ii) Kwamba siku ya kuweka sahihi mkataba huu, Mpangaji atamlipa Mwenye nyumba kiasi cha shilingi za Kitanzania Milion nne na laki mbili yaani (**TSH: 4,200,000/=**) ikiwa ni kodi ya nyumba kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia tarehe ya kuweka sahihi mkataba huu.
- (iii) Kwamba gharama za umeme, maji safi na maji taka, usafi wa nyumba na mazingira kwa ujumla zitakuwa ni juu ya mpangaji.
- (iv) Kwamba mpangaji hataruhusiwa kufanya marekebisho yoyote ya kiufundi kwenye nyumba bila ya kuwasiliana na /au kukubaliana na Mwenye nyumba tena kwa maandishi.
- (v) Mwenye nyumba anaweze kuingia ndani ya nyumba kwa ukaguzi wa kitu chochote na au matengenezo ya aina yoyote, baada ya kutoa taarifa ya siku tatu kwa mpangaji.

- (vi) Kwamba kila upande unaweze kusitisha au kuendelea na mkataba huu atatakiwa kutoa notisi ya mwezi mmoja kwa upande mwingine.
- (vii) Kwamba atakaevunja mashariti ya mkataba huu atatakiwa kulipa fidia ya gharama zote sawa na muda wa mkataba ulivotakiwa kuisha
- (viii) Kwamba mkataba huu utakuwa wa mwaka mmoja pande zote zaweza kurudia tena mkataba huu kwa makubaliano ya pande zote mbili na kwamba endapo mpangaji atapenda kurudia mkataba huu pindi kipindi kitakapokoma, itabidi atoe taarifa ya miezi mitatu kabla kwa Mwenye Nyumba.

Kwamba pande zote mbili zimekubaliana na masharti tajwa hapo juu na wanathibitisha nia na madhumuni yao ya kufuata maelekezo na /au masharti tajwa hapo juu kwa kuweka sahihi mkataba huu kama ilivyo hapa chini:

**IMESAINIWA na KUTOLEWA hapa DAR-ES-SALAAM**  
**EMMANUEL MSIGWA ambaye namfahamu/**  
**ametambulishwa**  
kwangu na Ndg. EMMANUEL MSIGWA  
leo tarehe 01, mwezi 02 2026.



**MWENYE NYUMBA**

**IMESAINIWA na KUTOLEWA hapa DAR-ES-SALAAM**  
na **MSIGWA INVESTMENT LIMITED** ambaye  
Namfahamu/ametambulishwa  
kwangu na Ndg. MSIGWA INVESTMENT LIMITED  
leo tarehe 01, mwezi 02 2026.

  
**MPANGAJI**

**MBELE YA.**

JINA:

CHEO:

TAREHE:

SAHIHI:

**KAMISHINA WA VIAPO**

Angela Mwaga  
Wakil  
11/02/2026  
AM

